Aidha, madeni yote ya makampuni husika tuliyoyanunua, tuliyarithi kama Taifa Group na tunaendelea kuyalipa.

Tunapenda kusisitiza kwamba miamala yote hii ilifanywa kwa kuzingatia kanuni na sheria za ndani ya nchi na za kimataifa zinazohusu manunuzi ya hisa za kampuni. Hivyo, kila hatua ilifanyika kwa uwazi, kwa mujibu wa sheria, na kwa kuzingatia malengo mapana ya maendeleo ya taifa letu la Tanzania.

TAIFA GROUP NA MAKAMPUNI YAKE TANZU, ITAENDELEA KUYAZINGATIA MAENEO MUHIMU YAFUATAYO:

1. Kuibadilisha Tancoal kuwa kielelezo na mfano bora wa uendeshaji wa migodi ya aina hiyo na hivyo, kuwa fahari kwa taifa letu.Tunajivunia kwamba kampuni yetu imeendelea kulipa mishahara ya wafanyakazi ambao hivi sasa wanashughulika na uhifadhi na utunzaji wa mgodi (care and maintenance) kabla ya uzalishaji kuanza rasmi. Shughuli hizo zisipofanyika mgodi huharibika. Wakati tunanunua hisa za TANCOAL, IEC walikuwa wameanza kusitisha shughuli za uchimbaji na hivyo, wafanyakazi wengi walikuwa hatarini kupoteza ajira zao laiti kama tusingezinunua hisa hizo. Aidha, tumelipa madeni ya muda mrefu tuliyoyarithi na tunatarajia kuanza rasmi uzalishaji pindi makubaliano ya wanahisa yatakapokamilika.

2. Kuyaendeleza mafanikio ya WDL licha ya ushindani tunaoupata kutoka kwa almasi zinazozalishwa katika maabara (synthetic diamonds). Tunajivunia kwamba kupitia uwekezaji wa kampuni yetu, WDL imeweza kuendelea na shughuli za uzalishaji baada ya kuwa imesitisha shughuli hizo huko nyuma. Aidha, tumewekeza kwa kiasi kikubwa katika shughuli za utafutaji wa maeneo mapya ya uchimbaji na hivyo, kuongeza muda wa maisha ya mgodi huo (life of mine).

TAHADHARI
Kusambazwa kwa makusudi kwa taarifa zisizo sahihi kuna madhara halisi na makubwa sio tu kwa kampuni zetu, viongozi na wafanyakazi wetu bali pia, kwa washirika wetu na jamii tunazozihudumia katika maeneo husika. Hivyo, jitihada za kuzichafua kampuni zetu hizi kwa kupotosha ukweli, ni jambo lisilokubalika na tunakusudia kuchukuwa hatua za kisheria dhidi ya wapotoshaji wote ndani na nje ya nchini yetu ya Tanzania.

Dr. Timothy Kyepa, LLD
Kwa Niaba ya Bodi ya Wakurugenzi,
Taifa Group Limited